# Nyoka Adhihirishwa

## *Katika Ushindi wa Kanaani*



Adrian Ebens

# Nyoka Adhihirishwa katika ushindi wa Kanaani

Adrian Ebens

Kimechapishwa na

MARANATHA
MEDIA

maranathamedia.com
adrian@maranathamedia.com

# Yaliyomo

Kukabiliana na Uhalisia ........................................................................5

Suala Madhubuti ambalo Wote Lazima walikabili.........................................6

Uwasilishaji wa Mungu Visivyo na Shetani ..................................................8

Mpango Asilia wa Mungu wa Kumiliki Kanaani ...........................................9

Hofu ya Israel ya Mungu ............................................................................10

Wakati Muhimu na Waamaleki ...................................................................11

Upanga wa kurithiwa ..................................................................................12

Miaka Arobaini Baadaye…..........................................................................16

Musa Anaupiga Mwamba kwa Kutotii .........................................................18

Waisraeli wanakula Kiapo ..........................................................................18

Mungu Anawapa Israeli Walichotaka .........................................................20

Kuachiliwa kwa Sanamu ya Utisho.............................................................22

Hukumu Bila Huruma..................................................................................23

Mwanga wa Utukufu...................................................................................25

Kumuona Mungu katika Nuru ya Kristo .....................................................26

## Kukabiliana na Uhalisia

> Kumb 2:34 Tukatwaa miji yake yote wakati huo, tukaharibu kabisa kila mji uliokuwa na watu, pamoja na wanawake na wadogo; tusimsaze hata mmoja:

Ni vigumu kusoma mafungu ya maandiko kama haya bila tetemeko la hofu kukimbia nafsini mwako. Ingawa baadhi hupata njia ya kuhalalisha mauaji ya waume wapiganaji, haidhahaniwi kuwa na taswira ya askari wa Israeli akiwa na mtoto mchanga akitundikwa mwishoni mwa upanga wake. Sijui kukuhusu wewe, lakini kwangu huleta hisia ya kuchanganyikiwa kabisa. Kile ambacho hufanya hili mbaya zaidi ni kwamba Bibilia huonekana sio tu kusamehe matendo haya, bali pia kuwaagiza.

> Kumb 7:2 wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao:

> Yoshua 11:12 Tena miji yote ya wafalme hao, na wafalme wake wote, Yoshua akawatwaa, akawapiga kwa makali ya upanga, na kuwaangamiza kabisa; vile vile kama huyo Musa mtumishi wa Bwana alivyomwamuru.

> Yoshua 10:40 Basi Yoshua akaipiga nchi hiyo yote, nchi ya vilima, na nchi ya Negebu, na nchi ya Shefela, na nchi ya matelemko, na wafalme wake wote; hakumwacha aliyesalia hata mmoja; lakini akawaharibu kabisa wote waliokuwa wavuta pumzi, kama Bwana, Mungu wa Israeli, alivyoamuru.

Imesemekana kuwa istilahi kuwaangamiza kabisa au kile ambacho kinajulikana kama marufuku, kinaweza eleweka visivyo katika hali ambayo kama kundi la watu lingeondolewa ramani kabisa basi mbona utoe agizo la kutooana nao?

> Kumb 7:2-4 wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao; **(3) binti yako usimpe mwanawe mume, wala usimtwalie mwanao mume binti yake.** (4) Kwa kuwa atamkengeusha mwanao mume asinifuate, ili wapate kuabudu miungu mingine; ndipo itakapowaka hasira ya Bwana juu yenu, naye atakuangamiza upesi.

Utata wazi unaweza suluhishwa katika kuelewa kwamba Israeli walikuwa wameagizwa kutangaza amani katika mji na kama wangefanya amani mji ungefanywa sehemu ya Israeli na miungu yao na mfumo wa ibada ungeharibiwa.

> Kumb 20:10-11 Utakaposongea karibu ya mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. (11) Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia.

> Kumb 7:5 Lakini watendeni hivi; zivunjeni madhabahu zao zibomosheni nguzo zao, yakateni maashera yao, ziteketezeni kwa moto sanamu zao za kuchonga.

Ila hata kama tutaruhusu hoja hizi, bado zinaangukia bali kidogo kwa fundisho la Kristo.

> Matt 26:52 Ndipo Yesu akamwambia, Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga.

> Luka 9:54-56 Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize kama Eliya alivyofanya? (55) Akawageukia, akawakemea (akasema, Hamjui ni Roho wa namna gani mliyo nayo). (56) kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuangamiza roho za watu, bali kuziokoa wakaenda katika kijiji kingine.

## Suala Madhubuti ambalo Wote Lazima walikabili

Kwa kweli halipaswi kuwa jambo la kushangaza kwamba suala la kuelewa tabia ya Mungu lazima lihusishe vita vya akili vinavyoonyeshwa na vita vya Yakobo na Malaika. Yakobo hangetambua utambulisho wa yule ambaye alipigana naye. Alidhani kuwa Malaika alikuwa adui yake aliyetumwa kumwangamiza, wakati ambao kwa kweli ilikuwa Mkombozi wake mwenye upendo aliyetumwa kumwokoa.

> Ni Kristo ndiye alikuwa na Yakobo usiku wote, ambaye alipigana naye, na ambaye alimshikilia kwa uvumilivu hadi akambariki. {1SP 119.1}

Kulikuwa na sababu moja ambayo Yakobo alivumilia pambano na Kristo.

> Shetani alikuwa amemshtaki Yakobo mbele ya Malaika wa Mungu, akidai haki ya kumuangamiza kwa sababu ya dhambi yake; alikuwa

amemsongesha Esau ili kuwa juu dhidi yake; na wakati wa usiku mrefu wa pambano, Shetani alikusudia kulazimisha juu yake hisia za hatia yake, ili kumtamausha, na kuvunja kujishikilia kwake kwa Mungu. Wakati katika diki yake Yakobo alimukwamilia Malaika, na kufanya ombi kwa machozi, Mjumbe kutoka mbinguni, ii kujaribu imani yake, pia alimkumbusha dhambi yake, na akajaribu kumuepuka. Lakini Yakobo hangegeuzwa**. Alikuwa amejifunza kuwa Mungu ni mwenye huruma, na akajiweka katika rehema zake.** Aliashiria [202] tena kwa kutubu kwake kwa dhambi yake, na akaomba kukombolewa. Alipoangalia maisha yake, alielekezwa karibu na kukata tamaa; lakini alimshikilia Malaika kwa nguvu, na kwa kilio cha nguvu na kuomboleza alisihi ombi lake hadi likatimia.

Huo ndio utakuwa uzoefu wa watu wa Mungu katika pambano lao la mwisho na nguvu za uovu. Mungu atajaribu imani yao, uvumilivu wao, ujasiri wao katika uwezo wake wa kuwaokoa. Shetani atajaribu kuwatisha na mawazo kwamba hali yao haina matumaini; kwamba dhambi zao zimekuwa kuu haziwezi sameheka. Watakuwa na hisia za kina za mapungufu yao, wakitazama maisha yao tumaini lao litazimia. Lakini wakikumbuka ukuu wa rehema ya Mungu, na kutubu kwao kwa kweli, wataomba ahadi zake zilizotolewa kupitia kwa Kristo kwa wadhambi wasio na uwezo, wanaotubu. Imani yao haitazimia kwa sababu ombi lao halijibiwi mara moja. Watajishikilia kwa nguvu za Mungu, kama Yakobo alivyomshikilia Malaika, na lugha ya mioyo yao itakuwa, "Sikuachi, usiponibariki." PP 201,202

Wale tu ambao wanashikilia ufahamu kwamba Mungu wetu ni mwenye huruma ndio watakuwa na ujasiri wa kuvumilia na kupokea baraka za Kristo kama Yakobo alivyofanya. Mgogoro huu wazi ambao huzuka kutoka kwa visa vya Agano la Kale na kauli za Kristo katika Agano Jipya hufungua mlango katika mawazo yetu kwa mbegu iliyopandwa na Shetani kwamba Mungu sio mwenye huruma. Tunakabiliwa na utata wazi ambao utapelekea kwa vita virefu na Mkombozi wetu kama hatujajifundisha kujua kwamba Baba yetu ni mwenye huruma na tunaweza amini rehema zake. Chuki ambayo hukaa mioyoni itajidhihirisha katika kusoma kwa visa hivi. Watu kama Richard Dawkins, Stephen Fry na wengine walitoa ushahidi wa mbegu hii chungu ambayo ilizaliwa na uongo ambao Shetani alianzisha. Ni uongo ambao humwasilisha Mungu kama dikteta asiyekuwa na huruma ambao hupelekea kwa utekelezaji wake katika mawazo ya watu, kama mahubiri ya wakana-

mungu hawa wapya kwamba Mungu ni holela, mwenye vurugu, na katili huwafanya wengi waache kuamini uwepo wake hata hivyo.

Kinyume chake, baadhi wako tayari kutetea tabia ya Mungu kama Mwenye huruma kwa kuongezea, kama mama yetu Hawa, kwa kile Neno la Mungu linafundisha. Baadhi hushindwa na uongo katika umbo la kijumla ambao hufundisha kwamba wote wataokolewa. Wengine huchukua mtazamo wa juu na kutuma Agano la Kale kwa "kufanya bora jinsi iwezekanavyo kwa wakati." Njia yoyote ile ujasiri katika kusoma wazi Andiko hufutwa na nyoka anaruhusiwa kunyonga moyo kwa kamba zake za udanganyifu.

## Uwasilishaji wa Mungu Visivyo na Shetani

Tangu mwanzo Shetani amewasilisha tabia ya Mungu visivyo.

> Ufahamu wa watu wa Mungu umepofushwa, kwa sababu Shetani amepotosha tabia ya Mungu. Bwana yetu mwema na mwingi wa fadhili amewasilishwa mbele ya watu akivishwa sifa za Shetani, na wake na waume wale ambao wamekuwa wakitafuta ukweli kwa muda mrefu wamemuona Mungu katika nuru potofu ni vigumu kuondoa wingu ambalo huchujuka utukufu wake usionekane nao. 1SM 355

Imekuwa mbinu ya Shetani tangu mwanzo kumvisha Mungu na sifa zake mwenyewe ili kwamba watu wamkatae. Tunaona kazi ya Shetani katika mauaji ya wanawake na watoto katika Mapinduzi ya Ufaransa.

> Kule Arrasi hata rehema katili ya kifo cha haraka haikutolewa kwa wafungwa. Kote kutelemka hadi Loire, kutoka Saumur hadi baharini, kundi kubwa la kunguru na mwewe lilisherehekea miili iliyoachwa uchi, ikiwekwa katika hali dhahiri. **Hakuna rehema ilitolewa kwa jinsia au umri**. Kundi la vijana wachanga na wasichana wa umri wa miaka kumi na saba ambao waliuawa na utawala huu katili, yanaweza onekana na mamia. **Watoto waliotolewa kwenye matiti walirushwa kutoka upande mmoja hadi mwingine**. Kwa kifupi kipindi cha miaka kumi, umati wa wanadamu uliangamia.
>
> **Yote haya yalikuwa jinsi Shetani alitaka yawe**. Hiki ndicho kwa miaka mingi ametafuta kupata. Sera yake ni udanganyifu tangu mwanzo hadi mwisho, na kusudi lake imara ni kuleta kilio na uovu kwa wanadamu, kuumbua na kuharibu kazi ya Mungu, kupotosha lengo takatifu la ukarimu na upendo, na kwa hivyo kusababisha huzuni mbinguni. **Kisha kwa sanaa yake ya udanganyifu hupofusha**

> **mawazo ya wanadamu, na huwaongoza kuelekeza lawama ya kazi yake kwa Mungu, kana kwamba taabu hizi zote ni matokeo ya mpango wa Muumbaji**. GC 283,284

Ni Shetani ndiye hushawishi wanadamu kuua bila huruma bila kuzingatia jinsia wala umri. Jaribio kuu ni kujua jinsi ya kusoma Maandiko kwa uaminifu, bila kuyafurukuta, ili kudhihirisha uhalisia huu. Tukiwa makini, wakati mwingine Mkombozi wetu atakuwa kama adui yetu akitafuta kutudhuru, lakini kama tumejua rehema za Mungu, tutavumilia hadi tupokee baraka. Ni hisia yangu ya ndani kwamba kukosa kuelewa tabia ya Mungu wetu sawasawa itaruhusu Shetani kushinda dhidi ya wale ambao hawafanyi jitihada ya kujua ukweli. Hii ni kazi ya uharaka mkubwa kama tutatiwa mhuri wakati wa mvua ya uvuvio. Kama ilivyokuwa kazi ya kwanza ya Shetani kupotosha tabia ya Mungu, hivyo ujumbe wa mwisho kwa ulimwengu utakuwa ufunuo wa tabia ya upendo wake.

> Ni giza la kutomuelewa Mungu ndilo linalojaza ulimwengu. Watu wanapoteza ufahamu wa tabia yake. Imefahamika na kufasiriwa visivyo. Katika kipindi hiki ujumbe kutoka kwa Mungu utatangazwa, ujumbe wa kuangaza katika athari zake na kuokoa kwa nguvu zake. Tabia yake itafanywa ijulikane. Katika giza la ulimwengu nuru ya utukufu wake itamwagwa, nuru ya wema wake, rehema, na ukweli.
>
> Hii ndio kazi inayoorodheshwa na nabii Isaya katika maneno, "Wewe uuhubiriye Sayuni habari njema, Panda juu ya mlima mrefu; Wewe uuhubiriye Yerusalemu habari njema, Paza sauti kwa nguvu; Paza sauti yako, usiogope; Iambie miji ya Yuda, Tazameni, Mungu wenu. Tazameni, Bwana Mungu atakuja kama shujaa, Na mkono wake ndio utakaomtawalia; Tazameni, thawabu yake i pamoja naye, Na ijara yake i mbele zake." Isaya 40:9,10.
>
> Wanaongojea kuja kwa Bwana harusi watawaambia watu, "Tazameni Mungu wenu." Mionzi ya mwisho ya nuru ya rehema, ujumbe wa mwisho wa rehema kutolewa kwa ulimwengu, ni dhihirisho la tabia Yake ya upendo. COL 415

## Mpango Asilia wa Mungu wa Kumiliki Kanaani

Kuhusiana na kumilikiwa kwa Kanaani na Waisraeli, Bwana aliwaambia jinsi hili litatekelezwa:

> Kut 23:27-30 Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. (28) Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti, watoke mbele yako. (29) Sitawafukuza mbele yako katika mwaka mmoja; nchi isiwe ukiwa, na wanyama wa bara wakaongezeka kukusumbua. (30) Nitawafukuza kidogo kidogo mbele yako, hata utakapoongezeka wewe, na kuirithi hiyo nchi.

Hapa hakujatajwa matumizi ya upanga. Israeli walikuwa wameponea Misri na wakaona Wamisri wakishindwa bila matumizi ya upanga hata mara moja.

> Bwana kamwe hakuwa amewaamuru 'mpande mkapigane.' **Haikuwa kusudi lake wamiliki nchi kwa vita**, bali kwa utiifu wa dhati kwa amri zake. PP 392

> Walipokuwa mwanzo wanajiandaa kuingia Kanaani, shughuli zilitekelezwa bila ugumu sana kama sasa. Mungu alikuwa amewaahidi watu wake kwamba **kama watatii sauti yake atatangulia mbele yao na kuwapigania; na pia atatuma [437] mavu kuwafukuza wakaazi wa nchi.** PP 436

## Hofu ya Israel ya Mungu

Katika kuwakomboa Israeli kutoka Misri, alikusudia wafahamiane naye na wajifunze kumuamini. Walipokuwa wakiishi Misri, Waisraeli walizungukwa na roho ya udhalimu. Katika mfano wa wana wa Waebrania wakitupwa kwenye mto, na maisha yao magumu Misri, wengi waliathiriwa na mtazamo kwamba Mungu ni katili kwamba anaweza wageukia wakati wowote na kuwaua. Tunaona hofu hii ikionyeshwa tangu mwanzo:

> Kut 14:11 Wakamwambia Musa, Je! Kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri?

Hofu inaturudisha nyuma hadi kwa bustani ya Edeni, Shetani alipomshawishi Adamu kwamba Mungu aliposema kuwa hakika watakufa kwamba ni yeye alikuwa aje kuwaua.

> Mwanz 3:10 Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.

Israeli walificha hofu yao ya Mungu waliyefahamu katika kumlaumu Musa. Ila ilikuwa ushahidi wazi kwamba Musa hakuwatoa watu kwa uwezo wake mwenyewe. Shetani alikuwa akiwajaribu watu kufikiria kwamba Mungu alikuwa anataka kuwaua jangwani. Jaribio hili lingewezekana tu kwa sababu ya ufahamu wao potovu wa tabia ya Mungu. Hofu hii inazidi kukua kwa Waisraeli:

> Kut 16:3 Wana wa Israeli wakawaambia, **Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri,** hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, tulipokula vyakula hata kushiba; kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote.

Waisraeli wanaonyesha hofu yao ya Mungu na wanasema wazi kuwa wanatamani wangekufia kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri badala ya kuvumilia hali yao ya sasa. Ni wazi kwamba hawakumwamini Mungu na mawazo yao yalikuwa yamepofushwa na Shetani kwa tabia yake ya kweli.

## Wakati Muhimu na Waamaleki

Katika sura ifuatayo ya Kutoka Waisraeli wanadhihirisha hata zaidi mawazo yao potovu kumhusu Mungu:

> Kut 17:3-4 Watu wakawa na kiu huko; nao wakamnung'unikia Musa, wakasema, Mbona umetupandisha kutoka Misri, kutuua sisi na watoto wetu na wanyama wetu kwa kiu? (4) Musa akamlilia Bwana, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe.

Wanaendelea kulalamika na kumlaumu Musa na kwa hivyo Mungu, kwa kutaka kuwaua. Mtazamo wao wa kisanamu wa Mungu katili unaanza kufasiri kwa vitisho vya kumuua Musa. Kwa kutazama dhana hii potovu ya Mungu katili wanabadilishwa kwa mfano huo na kupanga matendo ya ukatili dhidi ya mtu ambaye Mungu alitumia kuwakomboa kutoka Misri.

Manuguniko na malalamiko yaliyoendelea na kutomwamini Mungu kunamuweka katika nafasi ambayo hawezi kuwalinda. Wanamchagua Shetani kama bwana wao, na Shetani anadai kuwafikia na kuwaangamiza. Tunaona uhusiano baina ya malalamiko kuhusu maji na kuvamiwa na Waamaleki kama ifuatavyo:

> Kut 17:7-8 Akapaita mahali pale jina lake Masa, na Meriba; kwa sababu ya mateto ya wana wa Israeli, na kwa sababu walimjaribu Bwana,

> wakisema, Je! Bwana yu kati yetu au sivyo? (8) Wakati huo Waamaleki wakatokea, wakapigana na Israeli huko Refidimu.
>
> Bwana alijaribu imani ya watu wake, lakini hawakuvumilia jaribio. Walinugunika juu ya chakula, na maji, na wakalalamika kwa ajili ya Musa. **Kwa sababu ya kutokuamini kwao, Mungu aliruhusu adui zao kufanya** [229] **vita nao**, ili aweze kudhihirishia watu wake ambapo nguvu zao zinatoka. 1SP 228,229
>
> Kwa sababu ya kutotii na kuondoka kwa Mungu, waliruhusiwa kuletwa karibu na kupitia shida; adui zao waliruhusiwa kufanya vita nao, kuwanyenyekeza na kuwafanya wamtafute Mungu katika shida na dhiki zao. 2T 106.

Mateto ya wana wa Israeli yalimfungulia Shetani mlango wa kuchochea Waamalaki kuwavamia. Hili halingefanyika kama Israeli wangemwamini Bwana. Waamalaki wangehofia sana kuwaguza. Hakuna ushahidi kwamba Israeli walitubu dhambi zao dhidi ya Mungu. Walikuwa na mtazamo potovu wa Mungu kama katili mwenye dhamira ya kuwaua. Hakuna ushahidi wa shukurani kwa kupokea maji. Hakuna kuomba msamaha kwa Musa au kauli yoyote ya kumshukuru kwa kuomba maji. Hakuna chochote kimenakiliwa kuashiria hili. Waisraeli walikuwa wametishia kumuua Musa. Tunaweza fikiria ni jinsi gani hili lilimuumiza Musa? Angekaa katika mazingira yake tulivu ya nyumbani kwake jangwani akilinda familia yake na kuchunga kundi lake. Pia angehisi ukosefu wa shukurani wa kina waliokuwa wa kimwonyesha Mungu. Ingekuwa jaribio la kweli kwake. Kisha katika mchanganyiko huu wa mawazo, anapokea neno kwamba Waamaleki wanavamia na kunyakua wadhaifu. Kile ambacho kinafuata ni muhimu. Ni uamuzi ambao unafanywa katika hali ya kufisha moyo na msukumo.

> Kut 17:9 Musa akamwambia Yoshua, Tuchagulie watu, ukatoke upigane na Waamaleki; kesho nitasimama juu ya kilele kile, na ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu.

## Upanga wa kurithiwa

Haisemi, “Bwana akamwamuru Musa.” Haisemi kwamba Musa aliienda hekaluni na kumuomba Bwana. Inasema tu kwamba Musa alimwambia Yoshua aende akapigane. Ninapotazama taswira ya eneo la Musa akienda kwa Yoshua, kila kitu kinaenda kwa mwendo wa kujikokota na mawazo yangu

yanaelekezwa kwa usiku ambao Abrahamu alikuwa na mawazo ya kina kuhusu kile ambacho alikuwa ameshuhudia katika kumwokoa Loti.

> Abrahamu kwa furaha alirejea kwa hema yake na kundi lake, lakini mawazo yake yalisumbuliwa na fikara za kubughudhi. **Alikuwa mtu wa amani, akizuia uadui na ugomvi; na kwa hofu alikumbuka matukio ya mauaji aliyokuwa ameshuhudia**. Lakini mataifa ambayo alikuwa ameshinda majeshi yake bila shaka wangerudia mashambulizi ya Kanaani, na kumfanya chombo cha pekee cha kisasi chao. PP 136

Abrahamu, ambaye alishikilia nafasi sawa na Adamu, aliweka mwenendo wa tabia ya kurithiwa kwa vizazi vijavyo. Kuinuliwa kwa upanga na Abrahamu kungesababisha kitisho cha giza kuu kuanguka juu ya kizazi chake, na aliionja usiku huo wa hofu alipotafakari siku za kutisha za usoni kwa kuchukua upanga mikononi mwake. Mawazo yangu yanahamishwa hadi katika kijiji cha Shekemu, ambapo upanga unapasuka katika mikono ya wajukuu wa kuu wa Abrahamu Lawi na Simeoni katika kulipiza kisasi kwa dada yao aliyenajisiwa.

> Mwanz 34:25-29 Ikawa siku ya tatu, walipokuwa wakiumwa sana, wana wawili wa Yakobo, Simeoni na Lawi, nduguze Dina, wakatwaa kila mtu upanga wake, wakaujia mji kwa ujasiri, wakawaua waume wote. (26) Wakawaua Hamori, na Shekemu mwanawe, kwa makali ya upanga, wakamtwaa Dina katika nyumba ya Shekemu, wakatoka. (27) Wana wa Yakobo wakawajilia hao waliouawa, wakauteka nyara mji kwa sababu wamemharibu umbu lao. (28) Wakachukua kondoo zao, na ng'ombe zao, na punda zao, na vitu vilivyokuwamo mjini, navyo vilivyokuwako kondeni. (29) Wakatwaa na mali zao zote, na watoto wao wote, na wake zao, na vyote vilivyokuwamo nyumbani mwao wakavichukua mateka.

Mbegu ya tendo la Abrahamu la kuokoa mpwa wake inapasuka kwa kipimo kikubwa katika maisha ya Lawi na Simeoni wakisaidiwa na udanganyifu wa ndugu zao wengine katika kuwaagiza Washekemu watahiriwe. Kweli Yakobo angeomboleza kwamba wanawe watanuka machoni pa Wakanaani na Waperezi na kwamba, kama walivyokuwa wamechukua upanga, upanga ungewafuata katika vizazi vyote. Tunashuhudia athari za wana wa Lawi wakipeana kisa cha baba yao aliyeinuka kwa niaba ya dada yake na kuwaua Washekemu? Je, baadhi ya wana wa Lawi watajaribiwa kujivunia kile ambacho baba yao alikuwa amefanya katika kuokoa dada yake? Shetani hatawapendekezea kwamba alitakaswa katika matendo yake kama njia ya kujilinda? Si kukubali tafsiri hii ya kisa itakuwa rahisi kuliko kuelezea kwamba

baba yako wa awali alikuwa muuaji wa kumwaga damu na kubeba aibu ya hili katika vizazi vyote?

Yote ya kisa hiki sasa yanatembea katika nyayo za Musa kuelekea kwa Yoshua. Mawazo yako yanaelekezwa kwa awali katika maisha ya Musa. Jaribio sawa la kulinda "mmoja wetu" lilikuwa limekuja awali kwa Musa kwa umbo la mtumwa wa Misri akimpiga mmoja wa jamaa yake. Kisha wito wa kimya wa Baba yake Lawi unazuka kwa ghadhabu; upanga unainuliwa na hasira inaridhishwa.

> Musa aliharakisha sana katika kumuua Mmisri. Alidhani watu wa Israeli walielewa kwamba riziki ya Mungu ya kipekee ilikuwa imemuinua ili kuwakomboa. **Lakini Mungu hakupanga kukamilisha kazi hii kwa vita, kama Musa alivyodhani, bali kwa uwezo wake mkuu, ili kwamba utukufu uwe ni wake pekee**. Ila hata tendo hili la haraka lilitawaliwa na Mungu ili kuafikia kusudi lake. ST Feb 19, 1880

Miaka arobaini jangwani ilikuwa imemweka Musa huru kutoka kwa jaribio la kulinda watu wake kupitia kwa uamuzi wake mwenyewe? Kuna uwezekano Musa alikuwa amejifunza kwamba Waamaleki tayari walikuwa wameua baadhi ya wanyonge kambini? Muda mfupi kabla ya kufa kwake Musa alikumbuka:

> Kumb 25:17-19 Kumbuka aliyokufanya Amaleki katika njia mlipokuwa mkitoka Misri; (18) jinsi alivyokukuta katika njia, akapiga katika watu wako walioachwa nyuma, wote waliokuwa wanyonge nyuma yako, ulipokuwa umechoka na kuzimia; wala asimche Mungu. (19) Basi itakuwa, hapo atakapokwisha kukupumzisha Bwana, Mungu wako, katika adui zako wote walio kando-kando, katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi uimiliki, ndipo uufute ukumbuko wa Amaleki chini ya mbingu; usisahau.

Je, haya yote yalikuja pamoja kama Shetani alivyopanga ili kuwaongoza Israeli tena kuchukua upanga, kwa hivyo kufanya Israeli kunuka machoni mwa ulimwengu? Je, Shetani alikuwa amepanga hili ili tabia ya Mungu iweze kupotoshwa katika vizazi vyote? Waisraeli wenyewe walipotosha tabia ya Mungu, hivyo inaweza kuwa ni huko kuchukua upanga tu kulikuwa udhihirisho wa Mungu ambaye Israeli walifikiria? Kama hawa walidhahania Mungu hangewapa hata maji wakati yalihitajika, anawezaje kuwa hata kwa kiwango kidogo anajali kufa kwao kwa mikono ya Waamaleki?

Roho ya unabii inatwambia kwamba kamwe Mungu hakukusudia kutumia vita kumiliki Nchi ya Ahadi. Hivyo basi ni salama kuhitimisha kwamba matendo haya yasiyoamuriwa na yasiyoombewa ya kuita Yoshua akapigane na Waamaleki kwa upanga sio yale ambayo alikuwa amepanga? Ni wazi katika pambano kuu ambalo lilitendeka na maombi ya muda mrefu ambayo yalihitajika ili kusaidia Israeli kuwashinda Waamaleki kwamba hiki sio kile ambacho Mungu alikusudia awali. Ila Mungu aliwaruhusu kutembelea katika njia hii kwa sababu wengi wao walifikiria Mungu kama mtu katili na wa vita. Shetani aliporuhusiwa kuwaua Wamisri wakati huo wote alikuwa akiwaambia Waisraeli kwamba Mungu wao alikuwa akifanya mambo haya. Kwa maelezo ya matukio ya mapigo ya Misri, tazama kijitabu "*Calvary in Egypt*".

Mara tu ukichukua hatua hii itakuwa vigumu sana kutofikiria kutumia upanga tena. Mungu aliwasihi baada ya matukio na Waamaleki kwamba alikuwa na mbinu tofauti ambayo haikuhitaji matumizi ya upanga (Kut 23:27-30), lakini hadi wakati ambao Israeli wangeona tabia ya kweli ya Mungu wangejaribiwa tena na tena kuutumia.

Katika kisa cha Kora, Dathani na Abiramu na wakuu wa mkutano 250 tunaona jinsi hofu hii ya Mungu ambaye anataka kuwaua jangwani inawaongoza kutafuta utawala mwingine tofauti na Musa na Haruni. Kisha walipofika katika mipaka ya Kaanani wanatoa ripoti ya uongo kuhusiana na nchi kwa sababu hawakuweza kuamini kwamba Mungu aliwapenda na angewatendea mema. Walipuuza ulinzi wake wote na utunzaji na wakaangazia chochote hasi. Shetani angewajaribu kwa urahisi kuhusiana na vitu hivi kwa sababu walimwamini Mungu ambaye alitaka kuwaua na angebadili hisia zake wakati wowote. Wakati wowote ambao Shetani aliruhusiwa kuvunja ua la ulinzi na kuwaumiza Waisraeli, angewaambia kwamba Mungu alikuwa anawaadhibu moja kwa moja kwa mikono yake mwenyewe. Ni jambo la kuhuzunisha jinsi gani kwa Mungu watu wake kuamini uongo kama huo kumhusu kwa hiari.

> Hes 14:2-3 Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili. (3) Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka; je! Si afadhali turudi Misri?

Hes 14:22-23 kwa sababu watu hawa wote, ambao wameuona utukufu wangu na ishara zangu, nilizozitenda huko Misri, na huko jangwani, **pamoja na haya wamenijaribu mara hizi kumi, wala hawakuisikiza sauti yangu;** (23) hakika yangu hawataiona hiyo nchi niliyowaapia baba zao, wala katika hao wote walionidharau hapana atakayeiona:

Wakati Israeli waliambiwa kwamba hawatapanda na kuimiliki nchi kwa sababu ya dhambi zao, waliasi tena na wakaamua kupanda na kupigana, wakati ambao Mungu hakuwa amewaamuru wapigane.

## Miaka Arobaini Baadaye…

Waisraeli walikuwa wamesema mara kwa mara kwamba walikuwa wanahofia kwamba Mungu angewaua jangwani. Kama tutakavyochunguza muda mfupi baadaye, Mungu aliruhusu mtazamo wao wenyewe wa Mungu kuwahukumu. Na kizazi kizima kikafia jangwani kwa mkono wa mwangamizi ambaye alikuwa amewadanganya kuingia katika ibada ya sanamu ya kuamini mungu ambaye alitaka kuwaua jangwani.

Ayubu 3:25 Maana jambo hilo nichalo hunipata, Nalo linitialo hofu hunijilia.

Ayubu alihofia sana kwamba janga lingempata. Inawezekana kwamba sehemu ya sababu ambayo haya yalitendeka ni kwa sababu ya hofu ambayo Ayubu alikuwa nayo? Hofu ya mara kwa mara ya Mpangilio Mpya wa Dunia na kambi za vifo inaweza hasa changia kwa kumruhusu Shetani kufanya hili litendeke?

Miaka arobaini ilipokuwa imepita na kizazi chote kilikuwa kimeisha kwa kifo chao, walifika tena kwenye mpaka. Dhambi za mababa bado zilikuwa kwenye midomo ya wana:

Hes 21:5 Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu.

Kadri walivyozidi na safari yao kwelekea kusini, njia yao ilipitia katika bonde lenye joto na changarawe, bila kivuli au mimea. Njia ilionekana kuwa ndefu na ngumu, na walikumbwa na uchovu na kiu. Kwa mara nyingine walishindwa kuvumilia jaribio la imani yao na uvumilivu.

**Kwa kuendelea kudumu katika upande wenye giza la uzoefu wao, walijitenga zaidi na zaidi kutoka kwa Mungu.** Walipoteza uonekano wa ukweli kwamba kwa manuguniko yao maji yalipoisha Kadeshi, wangepata njia kupitia Edomi. Mungu alikuwa amepanga mambo mazuri kwa ajili yao. Mioyo yao ingejazwa na shukurani kwake kwamba ameadhibu dhambi zao bila uzito. **Lakini badala ya hili, walijisifu mno kwamba kama Mungu na Musa hawangeingilia, sasa wangekuwa wamemiliki inchi ya Ahadi. Baada ya kujiletea matatizo wao wenyewe, wakifanya mzigo wao kuwa mgumu kuliko vile Mungu alikuwa amepanga, walishtaki bahati yao mbaya juu yake. Kwa hivyo wakapenda mawazo machungu kuhusiana na shughuli zake nao, na hatimaye wakakosa kuridhika na kila kitu**. Misri ilionekana kung'aa zaidi na ya kutamanika kuliko uhuru na nchi ambayo Mungu alikuwa anawapeleka.

Waisraeli walipoingiza roho ya kutoridhika, walikuwa huru kuona kasoro hata kwa mibaraka yao. "Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu."

Musa kwa imani aliweka mbele ya watu dhambi yao kuu. Ni nguvu za Mungu tu ndizo zilikuwa zimewahifadhi katika "jangwa lile kubwa lenye kitisho, lenye nyoka za moto na nge, nchi ya kiu isiyokuwa na maji." Kumbukumbu 8:15. Kila siku ya safari yao walikuwa wamehifadhiwa kwa muujiza wa rehema takatifu. Katika njia zote za uongozi wa Mungu walikuwa wamepata maji ya kutuliza kiu yao, mkate kutoka mbinguni wa kushibisha njaa yao, amani na usalama chini ya kivuli cha wingu mchana na nguzo la moto usiku. Malaika waliwahudumia walipokuwa wakipanda milima yenye miamba au kupitia katika njia nyembamba na mbovu za jangwani. Bila kujali ugumu ambao walikuwa wamepitia, hakukuwa mdhaifu hata mmoja katika daraja zao zote. Miguu yao haikuwa imevimba kwa safari yao ndefu, wala nguo zao hazikuwa zimezeeka. Mungu alikuwa amewaondolea wanyama hatari wasiwale na wataambazi wenye sumu kali wa mwituni na jangwani. Kama hata na ishara hizi zote za upendo wake bado watu waliendelea kulalamika, Mungu angeondoa ulinzi wake hadi waelekezwe katika kuthamini ulinzi wake wa rehema, na warejee kwake kwa kutubu na udhalilishaji. {PP 428.3}

## Musa Anaupiga Mwamba kwa Kutotii

Waisraeli walikuwa wakisonga mbali zaidi na Mungu, na kiwango chao cha kuthamini tabia yake kikapungua zaidi na zaidi. Baada ya miaka arobaini Israeli tena walipitia juu ya nchi hiyo hiyo kuhusiana na kulalamika kuhusu kuwa na maji ya kutotosha, na mara tena walitoa mwitikio sawa, ila wazi zaidi.

> Hes 21:5 Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani?

Shetani alikuwa akitenda kazi kwa Musa wakati huu wote akimhimiza aachane na madhara haya duni. Mungu alikuwa amemjaribu Musa juu ya suala hili kwa manufaa yake mwenyewe Musa alipokuwa Mlimani pamoja na Mungu na Wana wa Israeli walikuwa wanaabudu ndama wa dhahabu (Kutoka 32:9-14), na kwa shukurani Musa aliitikia Roho wa Kristo na kumwomba Mungu asamehe watu, jambo ambalo alifanya kwa wingi wa neema. Ila sasa, akiona kwamba Israeli walikuwa wabaya hata zaidi kuliko awali, Musa anaanguka katika majaribu.

> Hes 20:10-11 Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu? (11) Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia.

Musa alipoanguka katika majaribu, ilimpa Shetani fursa kuu ya kufikia mawazo ya Waisraeli. Alikuwa amewaombea  na kusimama kati yao na Shetani kwa njia nyingi sana. Ila hatua hii ilimpa Shetani faida. Shetani alifurahia kwa kuweza kunyakua maisha ya Haruni kama tokeo la kuanguka huku.

> Hes 20:24 Haruni atakusanywa awe pamoja na watu wake; kwa kuwa hataingia katika nchi niliyowapa wana wa Israeli, kwa sababu mliasi kinyume cha neno langu hapo penye maji ya Meriba.

## Waisraeli wanakula Kiapo

Akiwa na fursa kuu ya kufikia mawazo ya Waisraeli, Shetani aliwatia katika kuanza majadiliano na Mungu, Mungu ambaye walifikiria alipenda kuua watu.

Walikuwa wamevamiwa na kabila lingine kwa sababu ya dhambi zao, na sasa katika kukata tamaa kwao walikula kiapo:

> Hes 21:1-3 Na Mkanaani, mfalme wa Aradi, aliyeketi upande wa Negebu, alisikia habari ya kuwa Israeli alikuja kwa njia ya Atharimu; basi akapigana na Israeli, na watu kadha wa kadha miongoni mwao akawateka mateka. (2) **Basi Israeli akaweka nadhiri kwa Bwana akasema, Kama wewe utawatia watu hawa mikononi mwangu kweli ndipo mimi nitaiharibu miji yao kabisa.** (3) **Bwana akasikiza sauti ya Israeli,** akawatia Wakanaani mikononi mwao; nao wakawaharibu wao na miji yao kabisa; na jina la mahali hapo likaitwa Horma.

Mungu hakuwaagiza Waisraeli kuwaua adui zao. Mtazamo wao wa uongo wa Mungu uliwafanya waamini kwamba angewataka kufanya kiapo cha kiu ya damu kama hicho, na kwamba hiki kingepata idhini yake, na angewasaidia. Inasema kwamba Mungu aliisikia sauti yao. Mbona Mungu akaisikia sauti yao? Hili halitawafanya dhabiti katika wazo kwamba Mungu aliwataka kuua adui zao? Jibu linapatikana katika mfano wa talanta:

> Luka 19:20-23 Kisha akaja yule mtumishi mwingine akasema, 'Bwana, hii hapa fedha yako. Niliitunza vizuri kwenye kitambaa. (21) Nilikuogopa, kwa sababu wewe ni mtu mgumu. Unachukua ambapo hukuweka kitu na unavuna mahali ambapo hukupanda kitu. (22) "Bwana wake akamjibu, '**Nitakuhukumu kwa maneno yako mwenyewe, wewe mtumishi mwovu!** Kama ulifahamu kwamba mimi ni mtu mgumu, nichukuaye mahali ambapo sikuweka kitu na kuvuna mahali ambapo sikupanda, (23) kwa nini basi hukuweka fedha zangu kwa watoa riba ili nitakaporudi, nichukue iliyo yangu na riba yake?

Mtumishi mvivu alidhani Bwana kuwa mtu mgumu. Kulingana na imani hii, alipokea hukumu. Kama Andiko lisemavyo:

> Yakobo 2:12-13 Hivyo semeni na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru. (13) Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu.

Mungu aliruhusu mtu ambaye alikuwa na mtazamo wa uongo kumhusu kuhukumiwa kulingana na mawazo yake mwenyewe. Mungu hufanyaje hili?

> Gal 6:7 Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna.

> Kut 34:7 mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne.

> Wakati wazazi na viongozi wanapuuza jukumu la kuadhibu kosa, Mungu mwenyewe atachukua jambo hilo. Nguvu zake zitakuwa katika kiwango kilichotolewa katika uwepo wa uovu, hivyo mfululizo wa matukio utazuka ambayo yataadhibu dhambi kwa dhambi. PP 727

Mataifa yaliyozunguka Israeli yalikuwa yamevuka mipaka ya ulinzi wa Mungu. Israeli walikataa kukubali ukweli wa tabia ya Mungu ya upendo. Walisisitiza katika kufikiria kwamba alitaka kuwaumiza na kila mtu mwingine. Israeli walipofikia mahali pa kula kiapo na Mungu cha kuua maadui zao, aliisikiliza sauti yao, sio kama karama ya utiifu balia kuwaruhusu kuwa na mtazamo wao potovu wa Mungu na kuadhibu dhambi kwa dhambi. Alipatiliza uovu wa baba kwa wanao kama alivyosema atafanya. Kuruhusu Israeli kuwashinda adui zake katika muktadha huu ilikuwa Bwana kuwaruhusu kushikilia kwa nguvu imani yao kuwa Mungu ni muuaji. Alijaribu kwa muda mrefu kuwaonyesha tabia yake ya kweli ya upendo kwa kuwanyunyuzia mibaraka mingi lakini mwishowe aliwaruhusu kudumisha imani zao katili za uongo na kuacha wahukumiwe na hili.

## Mungu Anawapa Israeli Walichotaka

Kabla ya anguko la kwanza la Israeli katika mipaka ya Kanaani tunawapata Waisraeli wakilalamika kuhusu tamaa yao ya nyama. Wanalia katita hema zao kwa sababu wanataka nyama wale. Katika hatua hii Musa analalamika kwa Bwana kuhusu mzigo ambao angeubeba.

> Hes 11:10-11 Basi Musa akawasikia watu wakilia katika jamaa zao zote, kila mtu mlangoni pa hema yake; na hasira za Bwana zikawaka sana; Musa naye akakasirika. (11) Musa akamwambia Bwana, Mbona umenitenda uovu mimi mtumishi wako? Kwa nini sikupata neema machoni pako, hata ukanitwika mzigo wa watu hawa wote juu yangu??

Jaribio hili la Musa linadhihirisha vipengele katika tabia yake ambavyo bado vinaonyesha uelewa usio sawa wa tabia ya Mungu.

> Hes 11:14-15 Mimi siwezi kuwachukua watu hawa wote peke yangu, kwa kuwa ni mzigo mzito sana wa kunishinda. (15) Na kama ukinitenda

> hivi, nakuomba uniulie mbali, kwamba nimepata fadhili mbele ya macho yako; nami nisiyaone haya mashaka yangu.

Musa anamuomba Mungu amuue ili kumpumzisha kutoka kwa mzigo huu. Eliya alikuwa na uzoefu sawa katika kukabiliana na Yezebeli. Yeyote ambaye amehisi kulemewa kabisa na hali anaweza elewa hisia za Musa; ila zinadhihirisha ukosefu wa imani kwa Mungu na shughuli zake. Kumsaidia Musa Mungu aliamuru:

> Hes 11:16 Kisha Bwana akamwambia Musa, Nikusanyie watu sabini, miongoni mwa wazee wa israeli, ambao wewe wawajua kuwa ndio wazee wa watu hawa, na maakida juu yao; ukawalete hata hema ya kukutania, wasimame huko pamoja nawe. .

Ila haukuwa mpango asilia wa Mungu kutawaza watu hawa sabini.

> Mungu alimruhusu Musa ajichagulie watu waaminifu zaidi na wenye ufanisi kushiriki majukumu naye. Athari yao ingesaidia katika kutazama vurugu za watu, na kukomesha uasi; ila maovu mahututi sana hatimaye yalitokea kwa kupandishwa cheo kwao. **Kamwe hawangechaguliwa kama Musa angeonyesha imani sambamba na ushahidi ambao alikua ameona wa nguvu na uzuri wa Mungu**. Lakini alikuwa amekuza mzigo wake mwenyewe na huduma, karibu kupoteza uwezo wa kuona uhalisia kwamba alikuwa chombo tu ambacho Mungu alikuwa amefanya. Hakusameheka kwa kujiingiza, kwa kiwango kidogo, roho wa kunugunika ambayo ilikuwa laana ya Israeli. Kama angemtegemea Mungu kikamilifu, Mungu angeendelea kumuongoza na angempa nguvu kwa kila kilichotokea. PP 380

Moja ya masuala ya kwanza ambayo yalizuka kutoka kwa mchakato huu ni kwamba Haruni na Miriamu walihisi kudunishwa na Musa katika uteuzi wa wazee sabini bila kuhusishwa. Hili lilipelekea kwa matatizo zaidi.

> Baada ya Musa kumwambia Bwana kwamba hangeweza kuubeba mzigo wa watu peke yake, Mungu akamwagiza kuteua wazee sabini, na alikuwa ameweka ndani yao roho sawa aliyekuwa ndani ya Musa, Haruni na Miriamu walikuwa na wivu kwa sababu hawakuwa wamehusishwa katika suala hili. 1SP 285

Kisha Bwana aliwapa Israeli tamaa ya mioyo yao ya chakula cha nyama.

> **Katika hatua hii Bwana aliwapa watu kile ambacho hakikuwa kwa ubora wa uzuri wao, kwa sababu walihitaji**. Hawangenyenyekea

> kupokea kutoka kwa Mungu vitu ambavyo vingethibitishwa ubora wao tu. Walijipa manuguniko ya kiasi dhidi ya Musa, na dhidi ya Bwana, kwa sababu hawakupokea vitu ambavyo vingewaumiza. 1SP 284

Kwa namna sawa Mungu alisikiliza kiapo ambacho Israeli walifanya cha kuua Aradi mfalme wa Wakaanani. Aliwapa kile ambacho hakikuwa bora kwa uzuri wao kwa sababu walikitaka.

Hivyo tunaona katika uteuzi wa wazee sabini na katika kutuma kware, Mungu alikuwa akiwapa Israeli vitu ambavyo walihitaji lakini ambavyo alijua sio bora kwao.

## Kuachiliwa kwa Sanamu ya Utisho

Hoja moja muhimu inahusiana na kile ambacho Mungu aliwaambia katika Kutoka 23:27

> Kut 23:27 Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao.

Mataifa yaliyokuwa yakiwazunguka katika Kanaani yote yalikuwa na mtazamo wa Mungu ambaye analipiza kisasi na muuaji. Ukweli kwamba mataifa mengine yangewatoa watoto wao kafara kwa miungu ulidhihirisha jinsi walimtazama kwa hali ya ujeuri, uuaji wa miungu yao. Neno la utisho katika Kutoka 23:27 linaweza tafsiriwa kama sanamu, kama katika kisa cha Yeremia 50:38.

> Yer 50:38 Ukosefu wa mvua u juu ya maji yake, nayo yatakaushwa; maana ni nchi ya sanamu za kuchongwa, nao wameingiwa na wazimu kwa ajili ya **sanamu**.

Kwa vile matafa yaliabudu miungu ya kutisha na kifo, Mungu aliruhusu dhambi ya Israeli kuleta juu ya mataifa haya kile ambacho walihofu na kuamini. Katika kuzungumza kuhusu mataifa ya kipagani Paulo anasema:

> Rom 1:32 Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti, si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia wanakubaliana na wale wanaoyatenda.

Hisia ya hatia kama tokeo la dhambi za Wakaanani iliwafanya kuhofu kifo na maangamizi. Baada ya Shetani kuupata moyo wa Israeli katika kuamini kwamba Mungu aliwataka wauwe watu, basi alikuwa na uwezo wa kushawishi Israeli kuapa kuua mataifa haya kwa vile Mungu alikuwa ameacha kuwalinda kwa sababu kikombe cha uovu wao kilikuwa kimejaa. Hivyo kama Mungu alivyokuwa ametabiri, hofu ya miungu ya uongo waliokuwa wameabudu ilikuja juu yao. Lakini hili liliwajilia kupitia kwa Waisraeli, badala ya njia ya kujiangamiza wenyewe.

## Hukumu Bila Huruma

Moja wapo wa ishara dhabiti kwamba Mungu aliwapa Waisraeli kile ambacho walihitaji ni kauli hii katika Kumbukumbu 7:2.

> Kumb 7:2 wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao:

Agizo la kuangamiza kabisa maadui bila huruma, na kuwa bado katika uiano na mungu ambaye Israeli walikuwa wamamfikiria halikuwa tafakari la Mungu wa kweli wa Mbinguni. Bibilia inasema kwamba hukumu hotolewa bila huruma kwa wale ambao hawajaonyesha huruma.

> Yakobo 2:13Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu.

Fungu hili linaweza somwa kwa njia mbili. Wale ambao hawana huruma watawahukumu wengine bila huruma na pia wale ambao hawana huruma hawatapokea yoyote wanapohukumiwa. Wazo hili la haki bila huruma linaakisi mawazo ya Shetani.

> Uwezo wa kuhukumu wa Shetani utamwongoza katika kuanzisha nadharia ya haki isiyoendana na rehema. Hudai kuwasilisha kama sauti na nguvu za Mungu, madai kwamba maamuzi yake ni ya haki, ni safi na hayana kosa. Hivyo huchukua nafasi yake juu ya kiti cha hukumu na kutangaza kwamba mashauri yake hayawezianguka. **Hapa haki yake bila huruma huingia, haki bandia, adui kwa mawazo ya Mungu.** Ellen White, Letter 16a 1892

Maandiko yanadhihirisha kwamba daima Mungu ni mwenye huruma:

Kut 34:6 Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli…

1 Nyak 16:34 Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema; Kwa maana fadhili zake ni za milele.

Haki ya Mungu kamwe haitengwi na rehema yake. Huu ni mpango wa Shetani. Zingatia matukio ya kuangamizwa kwa Yerusalemu:

Wayahudi walikuwa wameghushi pingu zao wenyewe; walikuwa wamejijazia wenyewe kikombe cha kisasi. Katika uharibifu wote ambao uliwapata kama taifa, na katika vilio vyote ambavyo viliwafuata katika kutawanyika kwao, walikuwa tu wakivuna mazao ya kile mikono yao wenyewe ilikuwa imepanda. Nabii anasema: "Ee Israeli, ya kuwa wewe u kinyume changu mimi, kinyume cha msaada wako;" "maana umeanguka kwa sababu ya uovu wako." Hosea 13:9; 14:1. **Kuteseka kwao mara nyingi kunawasilishwa kama adhabu inayopatilizwa kwao kwa amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu. Ni kwa hilo basi mdanganyifu mkuu hutafuta kuficha kazi yake**. Kwa kukataa kwa ukaida upendo na rehema takatifu, wayahudi walikuwa wamefanya ulinzi wa Mungu kuondolewa kutoka kwao, na **Shetani alikuwa ameruhusiwa kuwatawala kulingana na mapenzi yake. Ukatili wa kutisha uliyotekelezwa katika [36] kuharibiwa kwa Yerusalemu ni onyesho la nguvu za kisasi za Shetani juu ya wale ambao hutii utawala wake.**

Hatuwezi jua tunadeni kiasi gani ya Kristo kwa amani na ulinzi tunaofurahia. Ni nguvu za uzuizi za Mungu zinazo kinga wanadamu kutoingia kikamilifu kwa utawala wa Shetani. Waasi na wasio na shukurani wana sababu kuu ya kushukuru kwa rehema na uvumilivu wa Mungu katika kuangalia uwezo katili na mbaya wa yule mwovu. Lakini wakati ambao wanadamu wanavuka mipaka ya uvumilivu takatifu, uzuizi huo huondolewa**. Mungu hasimami kuelekea mdhambi kama mtekelezaji wa hukumu dhidi ya uasi: lakini huacha wanaokataa rehema yake, wavune kile ambacho wamepanda**. Kila mwali wa nuru ambao umekataliwa, kila onyo ambalo limepuuzwa au kutosikilizwa, kila tamaa imetekelezwa, kila uasi wa sheria ya Mungu, ni mbegu imepandwa ambayo hutoa zao lake lisiloepukika. Roho wa Mungu, anaye endelea kukataliwa daima, hatimaye huondolewa kwa mwenye dhambi, na kisha hakuna nguvu inayosalia kuongoza hamu ya uovu wa moyo, na hakuna ulinzi kwa uovu na uadui wa Shetani. Uharibifu wa Yerusalemu ni onyo la kutisha na makini kwa wote wanaochezea

karama za neema takatifu na kukataa wito wa rehema takatifu. Kamwe hakukutolewa ushahidi wa maamuzi ya kina kwa chuki ya Mungu ya dhambi na kwa ghadhabu fulani ambayo itawaangukia wenye hatia. GC 35, 36

Katika wakati ambao Israeli walifanya kiapo kwa Mungu kuangamiza mfalme wa Wakaanani walikuwa wanaongozwa na roho wa Shetani. Walikuwa wamenugunika na kulalamika dhidi ya Mungu na kuasi dhidi yake kwa kila fursa. Mungu aliwaonya na kuwahimiza kufuata amri zake:

Kumb 4:1 Na sasa, Ee Israeli, zisikilizeni amri na hukumu niwafundishazo, ili mzitende; mpate kuishi na kuingia na kuimiliki nchi awapayo Bwana, Mungu wa baba zenu.

Kumb 8:1 Amri hii ninayokuamuru leo mtaishika kuitenda, mpate kuishi na kuongezeka, na kuingia katika nchi ile ambayo Bwana aliwaapia baba zenu; nanyi mtaimiliki.

Ila Israeli walikataa kumtii Mungu na kwa hivyo Shetani aliwezeshwa kutawala hamu zao za hukumu bila huruma. Mungu aliwapa kile ambacho walitaka hata kama haukuwa mpango wake. Pia aliyapa mataifa ya kipagani kile ambacho walihofu kwa vile hawakuwa wamelindwa tena, Shetani alitumia Israeli kuwaua Wakaanani. Kwa kufanya hivi angeweza kuongoza mamilioni kwa vifo vyao kupitia kwa uelewa wao wa uongo wa tabia ya Mungu kama yule ambaye huua na kuangamiza watu.

## Mwanga wa Utukufu

Tunapata mwanga wa mpango wa Mungu wa kukabiliana na adui zao bila silaha katika mafungu kama haya:

Yos 24:11-12 Nanyi mliuvuka Yordani, mkafika Yeriko; nao watu wa Yeriko wakapigana nanyi, Mwamori, na Mperizi, na Mkanaani, na Mhiti, na Mgirgashi, na Mhivi, na Myebusi; nami nikawatia mikononi mwenu. (12) Nikatuma mavu mbele yenu, waliowafukuza mbele yenu hao wafalme wawili wa Waamori, **si kwa upanga wako, wala kwa upinde wako.**

2 Nyak 20:17-23 Hamtahitaji kupigana vita, jipangeni, simameni, mkauone wokovu wa Bwana ulio pamoja nanyi, enyi Yuda na Yerusalemu; msiogope, wala msifadhaike; kesho tokeni juu yao; kwa kuwa Bwana yu pamoja nanyi. (18) Yehoshafati akainama kichwa,

> kifulifuli; wakaanguka mbele za Bwana Yuda wote na wakaao Yerusalemu, wakimsujudia Bwana. (19) Na Walawi, wa wana wa Wakohathi na wa wana wa Wakorahi, wakasimama ili wamsifu Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sauti kuu sana. (20) Wakaamka asubuhi na mapema, wakaenda nje katika jangwa la Tekoa; nao walipokuwa wakitoka, Yehoshafati akasimama, akasema, Nisikieni, enyi Yuda nanyi wenyeji wa Yerusalemu; mwaminini Bwana, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waamini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa. (21) Naye alipokwisha kufanya shauri na watu, akawaweka wale watakaomwimbia Bwana, na kumsifu katika uzuri wa utakatifu, wakitoka mbele ya jeshi, na kusema, Mshukuruni Bwana; kwa maana fadhili zake ni za milele. (22) Nao walipoanza kuimba na kusifu, Bwana akaweka waviziao juu ya wana wa Amoni, na Moabu, na wa mlima Seiri, waliokuja juu ya Yuda; nao wakapigwa. (23) Kwani wana wa Amoni na wa Moabu waliwaondokea wenyeji wa mlima Seiri kuwaulia mbali na kuwaharibu; nao walipokwisha kuwakomesha hao wakaao Seiri, wakajitia kuharibu kila mtu mwenziwe.

Hivyo Israeli walipowezeshwa kuchukua nchi ya Kanaani kwa vita sio kile ambacho Mungu alikuwa amekusudia awali. Kwa vile Israeli walikuwa wamezidi kuhofu kwamba Mungu alikuwa anajaribu kuwaua na walishuku upendo wake wa utunzaji, Shetani aliwezeshwa kuwapotosha katika kuapa kwa Mungu kuwachinja Wakaanani na mataifa mengine ya kipagani. Israeli walishindwa na ushindi wao na wakafanywa watumwa wa mtazamo wao wa uongo wa Mungu.

## Kumuona Mungu katika Nuru ya Kristo

Katika siku hizi za mwisho tumepewa fursa ya kuona tabia ya Mungu kama kweli ilivyo. Machoni pa Yesu Kristo tunaweza anza kufunua makusudi ya kweli ya Baba yetu wa mbinguni.

> Yote ambayo mtu anahitaji kujua au anaweza jua kumhusu Mungu yamedhihirishwa katika maisha na tabia ya Mwanawe… {8T 286.1}
>
> Tefu, mwenye huruma, na rehema, mwenye kuwajali wengine daima, Aliwakilisha tabia ya Mungu, na wakati wote alikuwa katika huduma kwa Mungu na mwanadamu. {8T 286.4}

Ni watu wangapi Yesu aliwaua kwa upanga? Ni wangapi alichoma kwa moto? Ni watoto wangapi alitundika kwa mkuki? Hakuna kabisa! Kwa wale wote

wanaosikiliza mawazo kwamba Mungu alikuja kuangamiza roho za watu kumbuka maneno ya Yesu:

> Luke 9:55-56 Akawageukia akawakemea (akasema, Hamjui ni Roho wa namna gani mliyo nayo). (56) kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuangamiza roho za watu, bali kuziokoa.

Kadri tunavyoendelea kuamini uongo kwamba Mungu mwenyewe atawaangamiza wale wanaomkataa, tutapata kwamba Yesu huja kwetu wakati wa matatizo ya Yakobo kama adui na tutamuacha aende kabla tupokee baraka zake. Wale tu wanaompata Baba yetu kuwa mwenye rehema kweli watawezeshwa kuendelea kusimama na kutiwa mhuri dhidi ya uongo wa Shetani kwamba Mungu ni jeuri tunayepaswa kuogopa. Itagharimu matukio ya matatizo ya Yakobo kuweka wazi kikamilifu uovu huu wa wanadamu dhidi ya Mungu; hofu hii ambayo humtunga Mungu kama muuaji binafsi kwa wale ambao hufikiria kinyume naye.

Shetani atakushinda katika ushindi wa Kanaani kwa upanga, au utaona Baba yetu wa rehema akiruhusu watu wawe na mapenzi yao na kufuata mwenendo wao hadi mwisho? Chagueni hivi leo mtakayemtumikia; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Mungu mwenye rehema daima, ambaye kwa vyovyote vile hawezi ondoa uovu bali ataruhusu ngano na magugu zifike wakati wa mavuno ili kwamba moyo wa kila mwanadamu udhihirishwe.

*Nyoka Adhihirishwa*

katika

# Ushindi wa Kanaani

Tunaunganisha vipi mauaji ya jumla ya taifa la Israeli kwa upanga dhidi ya maneno ya Kristo?

> …Kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga

Sio tu wanaume, wanawake na watoto pia:

> Kumb 2:34 Tukatwaa miji yake yote wakati huo, tukaharibu kabisa kila mji uliokuwa na watu, pamoja na wanawake na wadogo; tusimsaze hata mmoja:

Je Waisraeli walikuwa kwenye mtindo wa tabia ya Mungu kwa kweli? Mbona wakati mwingi walikuwa na hofu kwamba alikuwa amewaleta jangwani kuwaua? Je, giza kuu ambalo lilianguka juu ya Abrahamu lilihusiana kwa vyovyote vile na kuchukua kwake kwa upanga ili kuokoa mpwa wake na familia yake?

Mauaji ya Washekemu na Lawi na Simioni yanaathari yoyote kwa kiapo cha Israeli cha kuangamiza adui zao kabisa?

Unahitaji kujua? Kama haukutaka Kristo angeweza kuja kwako kama alivyofanya kwa Yakobo katika mashaka yake na kuonekana kama adui? Kwa kuamini tu kwa rehema ya Mungu ndio Yakobo alishinda kama Israeli wa kweli wa Mungu.